**HOTUBA YA MGENI RASMI, BALOZI MHANDISI JOHN W. H. KIJAZI, KATIBU MKUU KIONGOZI KWENYE MKUTANO WA 16 WA MWAKA WA WAHANDISI NA KILELE CHA SHEREHE ZA MIAKA HAMSINI YA KUUNDWA KWA BODI YA USAJILI WA WAHANDISI (ERB), KATIKA UKUMBI WA DIAMOND JUBILEE, DAR ES SALAAM,**

**TAREHE 05 SEPTEMBA, 2018**

---

*Mheshimiwa Elias John Kwandikwa,*

*Naibu Waziri wa Ujenzi;*

*Waheshimiwa Mawaziri;*

*Mheshimiwa Paul Makonda,*

*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mhandisi Joseph M. Nyamhanga,*

*Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi);*

*Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;*

*Mhandisi Prof. Ninatubu Lema,*

*Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;*

*Wajumbe wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;*

*Mhandisi Patrick Barozi,*

*Kaimu Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;*

*Wenyeviti na Wasajili wa Bodi mbalimbali;*

*Watendaji Wakuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali za Serikali;*

*Wahandisi wote wa fani mbalimbali mliohudhuria Mkutano huu;*

*Wageni kutoka nje ya Tanzania;*

*Wageni Wote Waalikwa;*

*Wanahabari wote;*

***Mabibi na Mabwana***.

Habari ya Asubuhi!

Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia kukutana kwa mara nyingine katika **Mkutano huu wa mwaka wa Wahandisi**, ikiwa ni pamoja na kuadhimisha kilele cha Sherehe za miaka hamsini tangu kuundwa kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi hapa nchini. Leo ni siku muhimu, sio kwa jumuiya yetu ya Wahandisi tu, bali pia kwa Taifa letu kwa ujumla, kwani ni dhahiri kuwa kila mtanzania anatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na Wahandisi wa fani mbalimbali katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Hongereni sana Wizara na Bodi kwa kuandaa tukio hili, na hongereni sana Wahandisi wote kwa ushiriki wenu katika tukio hili muhimu, lakini muhimu zaidi Hongereni kwa mchango wenu mkubwa mnaoendelea kutoa katika ujenzi wa Taifa letu.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Nichukue fursa hii kipekee, kuwatambua na kuwakaribisha wageni wetu kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Afrika Kusini, Ethiopia, Misri, Nigeria, Ghana, Norway na Jamhuri ya Korea. Kuja kwenu kwa wingi ni furaha kwetu kwani inadhihirisha mnavyoshirikiana na Wahandisi wenzenu wa hapa Tanzania.

Nawahakikishia kuwa nchi yetu Tanzania ni nchi yenye sifa ya **amani** na **utulivu**, na popote mtakapokwenda mtapokelewa kwa ukarimu na furaha na wananchi wetu. Hivyo basi, pamoja na shughuli iliyowaleta Tanzania ya kushiriki katika Mkutano wa Mwaka wa Wahandisi na kuadhimisha miaka

hamsini tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi, nawashauri pia baada ya ratiba hii mtafute muda wa kutembelea sehemu mbalimbali za Tanzania ili muone vivutio vingi vya Utalii vilivyopo nchini kwetu, vikiwemo baadhi ambavyo ni nadra kuviona mahali pengine popote duniani. Karibuni sana, na kwa muda wote mtakaokuwa hapa nchini mjisikie mko nyumbani.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Naipongeza sana Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa kutimiza miaka hamsini tangu kuundwa kwake. Kwa binadamu mwenye mwenendo mzuri anapofikisha umri wa miaka hamsini anaonekana mbele ya jamii kuwa ni mtu aliyekomaa kiakili, mwenye busara na uzoefu mkubwa wa mambo mbalimbali, na ni wa kutegemewa katika kutoa ushauri kwa wanaouhitaji. Vivyo hivyo, Bodi ya Usajili wa Wahandisi pamoja na Jumuiya ya Wahandisi Tanzania, kwa ujumla katika kipindi hiki cha miaka hii hamsini mmekomaa, mmeimarika na mnaendelea kuwa tegemeo kubwa kwa maendeleo ya Taifa letu. Hivyo Jumuiya ya Wahandisi wote wa Tanzania, pamoja na Bodi ya Usajili wa Wahandisi, mnastahili kusherehekea siku hii muhimu mkiwa kifua mbele na kujivunia mafanikio makubwa mliyoyapata katika kipindi cha miaka hamsini iliyopita. Hongereni sana.

Nafahamu kuwa sherehe hizi zilizinduliwa tangu mwezi Mei mwaka huu, kufuatia uzinduzi huo, na Bodi imefanya makongamano mbalimbali katika kanda zake zote zilizopo Tanzania Bara kwa lengo la kuwawezesha wahandisi wengi zaidi waliopo katika sehemu mbalimbali za nchi kupata fursa ya kushiriki katika maadhimisho haya.

Aidha, nafahamu kuwa katika Makongamano hayo, Wahandisi walipata fursa ya kutembelea baadhi ya miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali.

Naipongeza sana Bodi kwa kuandaa utaratibu huo mzuri, kwani kwa kupitia makongamano hayo, mmewawezesha wadau wengi kufahamu zaidi kazi kubwa inayofanywa na Serikali yao ya kujenga miundombinu wezeshi ya kiuchumi kila mahali katika nchi yetu. Aidha, wadau wamejionea wenyewe michango mbalimbali inayotolewa na ninyi Wahandisi katika kutekeleza kazi hizo ambazo zinaliletea Taifa letu maendeleo.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Uhandisi ni maendeleo na maendeleo ni uhandisi. Hakuna jinsi ambavyo Taifa lolote linaweza kutekeleza mipango yake ya maendeleo bila ushiriki wa Wahandisi. Moja ya kitu kinachotofautisha nchi zinazoendelea na zilizoendelea ni idadi ya wahandisi waliopo katika nchi hizo. Wakoloni (Wajerumani na Waingereza) waliujua ukweli huu ndio maana katika kipindi chote cha zaidi ya miaka 70 ya utawala wao, **hawakusomesha na kuandaa Wahandisi wazawa.** Walichojitahidi kufanya katika miaka yao michache ya mwisho kabla ya nchi yetu kupata uhuru ni kusomesha mafundi sanifu wachache. Jambo hilo lilifanyika kwa makusudi ili kuifanya nchi yetu na nchi nyingine za Afrika kuendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuendelea kuwategemea wao. Mathalan, wakati tunapata Uhuru, mwaka 1961, kulikuwa na wahandisi wawili **(2)** tu nchini ambao wala hawakusomeshwa na wakoloni. Lakini katika kipindi cha miaka 56 tangu baada ya nchi yetu kupata uhuru hadi sasa, Tanzania imeweza kusomesha Wahandisi zaidi ya **22,226.** Hii ni kutokana na sera na mipango sahihi ya Serikali ambayo inatambua umuhimu wa Wahandisi katika maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na jitihada hizo za kusomesha Wahandisi, ili kuweka usimamizi mzuri wa taaluma ya Uhandisi hapa nchini, Serikali ya awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ilipitisha Sheria Na. 49 ya mwaka 1968 iliyounda **Bodi ya**

**Usajili wa Wahandisi** kwa mara ya kwanza, ambacho ni chombo cha kusimamia na kuratibu shughuli zote za kihandisi nchini. Hatua hii ilichukuliwa kutokana na umuhimu wa Uhandisi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya nchi yetu.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Mada kuu mliyoichagua kwa ajili ya majadiliano yenu ya kitaaluma inayosema "**Miaka Hamsini ya Michango ya Wahandisi Katika Maendeleo ya Taifa letu: Mafanikio, Changamoto na Malengo ya Baadaye**" ni mada stahiki kabisa kwani mada hiyo imekuja wakati sahihi tunapotekeleza Sera ya Uchumi wa Viwanda pamoja na ujenzi/utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile Reli ya "Standard Gauge"; mradi wa kuzalisha umeme katika bonde la Mto Rufiji, Bomba la Mafuta kutoka Hoima, nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga na kadhalika. Ni dhahiri kuwa baadhi yenu ninyi Wahandisi wa Kitanzania tayari mnashiriki ama mchango wenu utahitajika katika kutekeleza miradi hii mikubwa siku zijazo.

Aidha, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi wamebainisha kwenye hotuba zao, katika kipindi cha uhai wa Bodi hii, tumeshuhudia ongezeko kubwa la miundombinu mbalimbali, ikiwemo **mtandao mkubwa wa barabara, majengo ya kisasa, viwanda, miundombinu ya umeme, madaraja, viwanja vya ndege, miundombinu ya reli, bandari, miundombinu ya maji, miundombinu ya TEHAMA** n.k. Katika miradi yote hii, wahandisi mmetoa mchango mkubwa sana katika kufanikisha ujenzi wa miundombinu hiyo.

Mashahidi wakubwa wa maendeleo haya ni Wananchi, hasa wale ambao umri wao ni mkubwa kwani wanakumbuka jinsi hali ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji ilivyokuwa duni hapa nchini miaka ya nyuma, maana ilikuwa

vigumu sana kusafiri kwenda kwenye baadhi ya mikoa kama vile Tabora, Lindi, Mtwara, Kigoma, Kagera, Rukwa na mikoa mingine. Wakati huo, takriban miaka 80 iliyopita, barabara kuu ya lami ilikuwa moja tu ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, madaraja mengi yalikuwa ya miti na mbao, barabara nyingi zilikuwa zinapitika kwa kipindi kifupi na kufungwa kipindi kirefu cha mwaka wakati wa msimu wa mvua, meli kubwa na ndege kubwa zilikuwa haziji nchini n.k.

Hali hii sasa imebadilika kabisa kwani leo hii unaweza kuendesha gari ndogo kutoka Kaskazini mwa Tanzania hadi Kusini bila kukwama popote. Haya ni maendeleo makubwa, na ninafarijika kusema kwamba katika miaka 50 ya uwepo wa Bodi hii, Wahandisi wa Tanzania kwa ujumla mmetekeleza majukumu yenu vizuri, licha ya changamoto mbalimbali za hapa na pale. Ni matumaini yangu kuwa kazi hiyo nzuri itaendelezwa ili katika miaka mingine 50 ijayo mafanikio yetu yawe makubwa zaidi.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Kama mnavyofahamu jitihada za kukuza uchumi wa nchi yetu zinaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 (*Tanzania Development Vision 2025*) ambayo inalenga **kupunguza umaskini wa kipato na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati (*middle income economy*) ifikapo mwaka 2025.** Ili kuongeza kasi ya kufikia lengo hilo, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imelenga kujenga uchumi wa viwanda kwa **kuhamasisha uendelezaji wa viwanda vilivyokuwepo na kuanzisha viwanda vipya**. Viwanda hivi vimekusudiwa kuleta maendeleo ya watu yaliyo jumuishi na endelevu, kwa kuwapatia fursa za ajira zitakazokuza kipato chao. Vilevile, viwanda hivyo vinakusudiwa kutumia rasilimali na malighafi zilizopo nchini, na hivyo kuchangia katika kukuza Pato la Taifa. Ni matarajio ya Serikali kuwa,

pamoja na kutoa fursa nyingi za ajira, viwanda vitakuwa chachu ya maendeleo kwa kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya masoko ya ndani na nje.

Mafanikio ya utekelezaji wa azma ya kujenga uchumi wa viwanda yameanza kuonekana kwani tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, viwanda vipya zaidi ya **3,504** vimeanzishwa. Ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya viwanda na uchumi vinakuwa endelevu, utekelezaji wa miradi hii ya viwanda unaenda sambamba na upanuzi zaidi wa miundombinu mingine muhimu.

Aidha, ili malengo ya nchi yetu yatimie, ni muhimu pia kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na **Rasilimaliwatu ya kutosha** inayohitajika, na yenye **viwango vya ujuzi** vinavyokubalika kimataifa, hususan wahandisi wenye weledi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye ya viwanda na miundombinu yake. Ni dhahiri kuwa, ujenzi wa viwanda na miundombinu mingine muhimu utafanikiwa iwapo utaenda sambamba na utayarishaji wa rasilimaliwatu wanaohitajika kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uzalishaji viwandani kama wahandisi, mafundi stadi na mafundi sanifu.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Najua ipo changamoto ya Wahandisi na Wataalam wengine wa kutoka nje kufanya kazi nyingi za Kihandisi nchini. Sote tunafahamu kuwa hakuna nchi ambayo itaendelezwa na wataalam wa kutoka nje. Hivyo, ni muhimu tukahakikisha kuwa Wahandisi wa kigeni wanatumika pale tu wanapohitajika, na hasa katika kujenga uwezo wa wataalam wetu wa ndani. **Hivyo, ni muhimu Bodi ya Usajili wa Wahandisi mnao wajibu wa kuhakikisha kuwa, sheria iliyounda Bodi hii inatekelezwa kikamilifu kuhusiana na ajira za wahandisi wageni**.

Vilevile, nafahamu kuwa ipo changamoto ya Wahandisi Wahitimu (*Graduate Engineers*) kutopata fursa za kutosha za kufanya mazoezi kwa vitendo mara baada ya kuhitimu ili wafikie ngazi ya kuwa Wahandisi Wataalam (*Professional Engineers*). Ninayo taarifa kuwa baadhi ya waajiri hutaka tu kuajiri wahandisi waliokwishaendelezwa kivitendo na kufikia kiwango cha kutambulika kuwa Wahandisi wataalam. Tabia hii imesababisha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutwishwa mzigo wa kugharamia mafunzo kwa vitendo ya wahandisi wahitimu. Kwa kuwa uwezo wa Wizara ni mdogo, Wahandisi Wahitimu wengi wanakosa nafasi ya kupata mafunzo. Niwaase waajiri wote wa wahandisi kuhakikisha wanaweka utaratibu wa kuajiri Wahandisi wahitimu na kuwajengea uwezo wakiwa kazini. Ieleweke kuwa hawa ndio nguvukazi yetu tunayoitegemea siku zijazo, hivyo kama makampuni ya hapa nchini hayatawajengea uwezo, ni nani atafanya hivyo?

Mheshimiwa Waziri, ni vizuri Wizara yako ikaweka **utaratibu madhubuti** utakaotumiwa na Taasisi zote zinazotekeleza miradi mikubwa ya kihandisi kuhakikisha kuwa **zinatoa nafasi** kwa wahandisi wanaojifunza kupata uzoefu. Jambo hili litasaidia katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inajijengea uwezo wa kuwa na wataalam wake wenye ujuzi wa kutosha siku zote. Upo umuhimu pia kwa Wizara na Bodi kuanzisha **mfuko mahsusi** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu. Kwa mfano, mnaweza kuweka utaratibu ambao waajiri wa Wahandisi watachangia mfuko huo. Fikirieni pia vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya mfuko huo.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Hatuna budi kufahamu kuwa, hivi sasa na huko tuendako michango ya wahandisi itahitajika zaidi kuliko miaka 50 iliyopita. Kama nilivyotangulia

kusema, katika miaka miwili na nusu tu iliyopita, viwanda vipya zaidi ya **3,504 vya ukubwa** tofauti vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, wawekezaji wengi zaidi wanaendelea kujitokeza kwa nia ya kuwekeza katika sekta ya viwanda hapa nchini. Uzalishaji viwandani utaendelea kuongezeka kutokana na kukua kwa soko kufuatia makubaliano na mikakati mbalimbali ya Kikanda ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). **Uwekezaji wote huu kwa vyovyote vile, utahitaji huduma za kihandisi kwa kiwango kikubwa**.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Kama nilivyosema awali, Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kujenga mazingira wezeshi ili kuhakikisha kuwa viwanda vilivyopo na vitakavyojengwa havikwami kutokana na matatizo ya upatikanaji wa mali ghafi, nishati, usafiri usio wa uhakika au ukosefu wa maji. Serikali imeweka mkazo katika baadhi ya miradi mikubwa na ya kimkakati ambayo imeanza na inaendelea kutekelezwa. Miradi hiyo inahusisha:

(i) Ujenzi wa reli ya kisasa (*Standard Gauge Railway)* na ukarabati wa reli zilizopo;
(ii) Undelezaji wa mtandao mkubwa wa barabara za lami;
(iii) Upanuzi wa bandari;
(iv) Uendelezaji wa mradi wa kufua umeme katika Mto Rufiji eneo la (*Stiegler's Gorge)* pamoja na miradi ya umeme Vijijini;
(v) Ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege;
(vi) Uboreshaji wa usafiri katika maziwa;
(vii) Upatikanaji wa maji ya kutosha mijini na vijijini;
(viii) Ujenzi na ukarabati wa vyuo vikuu, shule za sekondari, shule za msingi, na shule za awali; na

(ix) Hospitali za rufaa na vituo vya afya n.k.

Hivyo, ni muhimu Wahandisi wazawa mjipange kimkakati ili kushiriki ipasavyo katika fursa hizi na nyingine zitakazojitokeza, ikiwa ni pamoja na kushiriki kama wawekezaji katika Sekta ya Viwanda. Serikali ingependa kuona hilo linafanyika kwa kiwango kikubwa na Serikali itatoa ushirikiano wa kutosha katika kulifanikisha.

**Ndugu Wahandisi na Wageni Waalikwa,**

Napenda nimalizie hotuba yangu kwa kuwakumbusha baadhi ya mambo katika utekelezaji wa majukumu yenu. **Uhandisi ni taaluma na ina miiko yake**. Kwenda kinyume na miiko hiyo ni kuchafua sifa nzuri ya wahandisi na kuwafanya wananchi na Serikali kukosa imani kwenu kutokana na miradi kutekelezwa kwa kiwango duni na kisicholingana na thamani ya fedha iliyotumika (*Value for Money*).

Serikali ya Awamu ya Tano ina imani kubwa nanyi na inawategemea sana. Hivyo, nawaasa nyote kuwa macho na kudhibiti vitendo vinavyoweza kuchafua sifa nzuri ya taaluma ya Uhandisi. Baadhi ya vitendo hivyo ni **rushwa, kufanya kazi chini ya kiwango, uzembe katika usimamiaji wa miradi, miradi mingi kutokukamilika kwa wakati na mingine kutokukamilika kabisa na gharama kubwa zinazotozwa na wahandisi na wakandarasi.** Vitendo hivi vinaligharimu Taifa fedha nyingi na kurudisha nyuma maendeleo, kwani wakati mwingine Serikali hulazimika kurudia kutekeleza miradi ile ile baada ya muda mfupi badala ya kutumia fedha hizo kuendeleza miradi mingine mipya. **Bodi ya Usajili wa Wahandisi pamoja na Bodi nyingine zinazohusika mnao wajibu, kwa mujibu wa sheria zilizoanzisha Bodi zenu, kudhibiti vitendo hivi**

**visitokee miongoni mwa Wahandisi ama makampuni ya Kihandisi, na pale vinapotokea basi mchukue hatua kali dhidi ya wahusika**. Tekelezeni wajibu wetu wa kusimamia kikamilifu taalum ya Kihandisi bila kusita wala kulindana.

**Ndugu Viongozi, Wahandisi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**

Sherehe ya kutimiza miaka hamsini ni sherehe kubwa kwa taasisi yoyote, hivyo nami nimefarijika sana kuja kushiriki nanyi katika sherehe hii na kutoa mchango wangu katika mada inayoongoza sherehe hizi, na kusherekea pamoja nanyi japo kwa muda mfupi.

Kwa mara nyingine nwapongeza sana wote mlioshiriki katika kufanikisha tukio hili la kihistoria.

Baada ya kusema hayo, ninayo furaha kutamka kuwa **Sherehe ya Kutimiza Miaka Hamsini ya Kuundwa kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)na Mkutano wa 16 wa Mwaka wa Wahandisi** umefunguliwa rasmi.

***Asanteni kwa kunisikiliza***